KUCHUNGUZA DHAMIRA YA MAPENZI NA FANI KATIKA KITABU CHA MAPENZI BORA CHA SHAABAN ROBERT

FATMAH TWALIB ZAHOR

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2017

UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma kazi hii na anaidhinisha ikubaliwe kwa utahini na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania yenye mada: **“Kuchunguza Dhamira ya Mapenzi na Fani Katika Kitabu cha Mapenzi Bora cha Shaaban Robert”,** na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa shahada ya M.A Kiswahili ya Chuo kikuu Huria.

…….

Sheikh, Dkt, Prof.T.S.Y.Sengo

(Msimamizi)

Tarehe……

HAKI MILIKI

Sehemu yoyote yatasnifu hii, hairuhusiwi kubadilishwa au kuigwa kwa kutumia njia yoyote ile bila ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

TAMKO

Mimi **Fatmah Twalib Zahor**, ninathibitisha kwamba tasnifu hii, iitwayo "Kuchunguza dhamira ya mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora*" ni kazi yangu mwenyewe na kwamba haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada nyingine yoyote.

……

Saini

…….

Tarehe

TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa, **Baba Twalib Zahor Mbottoni** na **Mama Nafsah Seif Nindi** kwa kunilea vema na kunipa maadili bora yanayoridhiwa na Allah (S.W.T).

SHUKRANI

Ninayofuraha kubwa kabisa kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili, kunipa afya, nguvu na uwezo wa kuweza kuifanya kazi hii mpaka kuimaliza.

Pili, natoa shukrani zangu za dhati na za pekee kwa msimamizi na mwalimu wangu Sheikh, Dkt, Prof .T.S.Y.M. Sengo, ambaye amefanya kazi kubwa ya kuniongoza, katika uandishi wa tasnifu hii mpaka kukamilika. Kutokana na busara na na hekima zake hakuchoka kunikosoa na kunielekeza. Kwa hakika sina cha kumlipa mwalimu wangu ila namuomba Allah (S.W.T) azidi kumpa afya na nguvu, pamoja na mwisho mwema "Amin."

Tatu, natoa shukrani zangu za dhati kwa mama yangu aliyenizaa kwani hakuchoka kunihimiza, kunipa moyo na kuwalea watoto wangu kwa mapenzi makubwa kipindi chote cha masomo yangu. Sina cha kumlipa mama ila kumuombea siku zote, Allah ampe umri wenye afya njema na mwisho mwema "Amin".

Nne, nitakuwa mkosefu wa fadhila nisipomshukuru mume wangu mpenzi, kwanza kwa kuniruhusu kusoma ,pia kwa kuwa bega kwa bega na mimi tangu mwanzo hadi mwisho wa masomo yangu. Kwa hakika amenipa msaada mkubwa wa hali na mali, siwezi kusahau busara zake za kunihimiza pindi ninapokata tamaa au kuchoka. Sina cha kumlipa ila ninamuombea sana afanikiwe katika shughuli zake ,ajaliwe afya njema na Allah (S.W.T) amzidishie huruma ,busara na mapenzi "Amin"

Tano,natoa shukran zangu za dhati kwa kaka yangu Jamal Adam kwa kunishauri kuendelea masomo na kunipa msaada wa hali na mali na hatimaye kuweza kumaliza masomo yangu. Kwa kweli sina cha kumlipa ila namuombea afya njema na mafanikio katika shughuli zake za kila siku

Sita, natoa shukrani zangu za dhati kwa wanangu wapenzi Ahmed Omar Mohamed na Azzah Omar Mohamed kwa uvumilivu wao mkubwa walioufanya nikiwa katika masomo yangu kwani walikosa kukaa na mimi kwa muda mrefu, na waliniona kwa muda mchache, Allah awakuze vyema "Amin". Na pia shukrani zangu za dhati kwa mdogo wangu mpendwa Salama Twalib kwa kuwa karibu na mwanangu Azzah kipindi chote cha masomo yangu, Allah amzidishie mapenzi na amjaalie kila lililo la kheri "Amin".

Mwisho,napenda kutoa shukurani zangu za pekee kwa wataalamu wote wa idara ya fasihi kwa maoni yao, mwongozo wao na busara zao. Si rahisi kuwataja wote lakini kwa niaba yao naomba niwataje wafuatao:-Profesa Emmanuel Mbogo na Daktari Mohammed Omar, ninawaambia asanteni sana.

IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza dhamira ya mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert. Ili kutimiza lengo kuu, kulikuwa na malengo mahsusi matatu; Kuainisha dhamira za mapenzi katika kitabu cha *Mapenzi Bora*, kuchambua dhamira za mapenzi zilizojitokeza katika kitabu cha *Mapenzi Bora* kuchunguza vipengele vya fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora.* Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na mbinu ya maktabani. Data hizo zilikusanywa na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Matokeo ya kiutafiti yanaonesha kuwa katika kitabu cha mashairi cha *Mapenzi Bora* mtafiti ameainisha dhamira ya mapenzi katika makundi saba ambayo ni mapenzi ya Kimungu Mungu, mapenzi ya mitume, mapenzi ya sisi kwa sisi, mapenzi ya yasiyoangalia kabila, taifa wala rangi, mapenzi ya kupenda majirani na marafiki, mapenzi ya kudumu na mapenzi ya kupenda nchi. Dhamira hiyo ya mapenzi katika mafungu hayo saba, zinasisitiza mapenzi yaliyo ya ukweli ambayo yatasababisha kuwepo kwa amani na upendo miongoni mwa watu. Mapenzi ya kusaidiana katika shida na raha. Mapenzi ya kuvumiliana na kufanyiana subira katika matatizo, mapenzi ya kutokubaguana kwa kuangalia kabila, cheo, dini wala uzuri wa mtu, hayo ndiyo mapenzi ya kweli. Kwa upande wa fani vilivyoangaliwa ni vipengele vya lugha na muundo. Kuna tamathali za usemi nyingi ambazo ni takriri, tashibiha, tashihisi, sitiari, kejeli na taswira, pia kwa upande wa muundo ni tarbia, mizani nane, urari wa vina na mizani na kituo bahari.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ii

HAKI MILIKI iii

TAMKO iv

TABARUKU v

SHUKRANI vi

IKISIRI viii

SURA YA KWANZA 1

1.0 UTANGULIZI KWA UJUMLA 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Usuli wa Tatizo 1

1.3 Tatizo la Utafiti 2

1.4 Malengo ya Utafiti 2

1.4.1 Lengo kuu la Utafiti 2

1.4.2 Madhumuni Maalumu ya Utafiti 2

1.4.3 Maswali ya Utafiti 3

1.5 Umuhimu wa Utafiti 3

1.6 Mipaka ya Utafiti 4

1.7 Vikwazo vya Utafiti 4

1.8 Utatuzi wa Vikwazo 4

1.9 Wasifu wa Shaaban Robert 5

1.10 Hitimisho 6

SURA YA PILI 7

2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA . 7

2.1 Utangulizi....7
2.2 Pengo la Kimaarifa....9
2.3 Dhana ya Ushairi....9
2.4 Dhana ya Dhamira....10
2.5 Dhana ya Fani....11
2.6 Tamathali za Usemi....11
2.7.1 Tashibiha....12
2.7.2 Takriri....12
2.7.3 Tashihisi....12
2.7.4 Sitiari....13
2.7.5 Taswira....13
2.8 Mkabala wa Kinadharia....14
2.8.1 Nadharia ya Fani....14
2.8.2 Nadharia ya Fasihi na Jamii....15
2.9 Hitimisho....16
SURA YA TATU....17
3.0 MBINU ZA UTAFITI....17
3.1 Utangulizi....17
3.2 Eneo la Utafiti....17
3.3 Watafitiwa....17
3.4 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli....18
3.4.1 Kundi Lengwa (Sampuli na Usampulishaji)....18
3.4.2 Sampuli Nasibu....18
3.5 Aina za Data Zilizokusanywa....19

3.5.1 Data za Msingi 19
3.5.2 Data za Upili 19
3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data 20
3.6.1 Mbinu ya Usomaji Makini 20
3.6.2 Mbinu za Maktabani 20
3.7 Vifaa vya Utafiti 20
3.8 Uchambuzi wa Data 21
3.9 Hitimisho 21
SURA YA NNE 22
4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA 22
4.1 Utangulizi 22
4.2 Kuainisha Dhamira za Mapenzi Katika Kitabu cha Mapenzi Bora 22
i) Mapenzi ya Mungu 22
4.3 Kuchambua Dhamira za Mapenzi Katika Kitabu cha Mapenzi Bora 23
4.3.1 Mapenzi ya Mungu 23
4.3.2 Mapenzi ya Mitume 24
4.3.3 Mapenzi ya Sisi kwa Sisi 24
4.3.4 Mapenzi Yasiyoangalia, Kabila, Taifa wala Rangi 25
4.3.5 Mapenzi ya Kudumu 25
4.3.6 Mapenzi ya Majirani na Marafiki 26
4.3.7 Mapenzi ya Nchi 27
4.4 Uchambuzi wa Vipengele vya Fani Katika Kitabu cha Mapenzi Bora 27
4.4.1 Matumizi ya Tashibiha 28
4.4.2 Matumizi ya Takriri 29

4.4.3 Matumizi ya Tashihisi 30
4.4.4 Matumizi ya Sitiari 30
4.4.5 Matumizi ya Kejeli 31
4.4.6 Matumizi ya Taswira 32
4.5 Muundo/ Umbo la shairi 33
4.5.1 Idadi ya mshororo katika ushairi wa Mapenzi Bora 33
4.5.2 Vina na mizani katika ushairi wa Mapenzi Bora 34
4.5.3 Kituo Katika Ushairi wa Mapenzi Bora 35
4.6 Hitimisho 35
SURA YA TANO 36
5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 36
5.1 Utangulizi 36
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti 36
5.2.1 Kuainisha Dhamira Zilizojitokeza Katika Kitabu cha Mapenzi Bora 36
5.2.2 Uchambuzi wa Dhamira Zilizojitokeza Katika Kitabu cha Mapenzi Bora 37
5.2.3 Uchunguzi wa Vipengele vya Fani Katika Kitabu cha Mapenzi Bora 38
5.3 Mapendekezo 38
5.3.1 Mapendekezo kwa Wasomaji na Jamii kwa Ujumla 38
5.3.2 Mapendekezo kwa Serikali 39
5.3.3 Mapendekezo kwa Watafiti 39
MAREJELEO 40

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI KWA UJUMLA

1.1 Utangulizi

Sura hii ni sura tangulizi ambayo inabainisha na kueleza juu ya usuli wa tatizo, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti ,mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti,utatuzi wa vikwazo,wasifu wa Shaaban Robert na hitimishi.

1.2 Usuli wa Tatizo

Fasihi ni kazi ya sanaa inayotumia lugha kuwasilisha ujumbe kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo **(**Mulokozi na Sengo,1995). Kwa kutumia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi tunaweza kubadili mielekeo, mitazamo, tamaduni, imani, mila na desturi za jamii husika.

Fasihi simulizi inatusaidia kujifunza utamaduni wa umma, kuelewa misimamo, itikadi na mahitaji yao na kuwasaidia kuitumia fasihi yao na kuendeleza mapambano dhidi ya mazingira yao. Hivyo ni wazi kuwa fasihi simulizi huweza kuibua masuala mbalimbali yanayoibuka katika jamii na kuleta athari kwa jamii na kwa haraka zaidi (Mulokozi,1982). Fasihi simulizi ni utanzu wa fasihi ambao una tanzu nyingi. Moja ya tanzu zake ni ushairi. Shairi ni utungo unaotumia lugha ya mkato, mnato na mvuto katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii (Mulokozi na Kahigi,1979).

Topan, (1974), Shairi ni utungo unaoelezea hisia za ndani za mwanadamu kwa mpangilio fulani wa maneno. Kwa kawaida kazi za fasihi kwa upande wa ushairi pia zinakuwa na dhamira mbalimbali zinazoakisi jamii kwa ujumla. Jamii inakuwa na

mapenzi, uhasama, husuda, furaha na hata uadui. Kwa hiyo yaonyesha wazi kwamba kazi za fasihi dhima yake ni kufikisha ujumbe kwa jamii kupitia dhamira zake mbalimbali ikiwemo dhamira ya mapenzi.

Hivyo basi, utafiti huu unachunguza dhamira ya mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora*.

1.3 Tatizo la Utafiti

Shaaban Robert ni miongoni mwa washairi wa ushairi wa Kiswahili ambaye amejipatia sifa kubwa kutokana na umahiri wake wa utunzi wa kazi zenye mvuto mkubwa kwa watu.

Katika kitabu chake cha *Mapenzi Bora* hakuona ajizi kutunga beti zipatazo 700 ambazo zinahusu mapenzi. Hivyo, mtafiti kutokana na umuhimu wa kitabu hicho, ameona achunguze dhamira ya mapenzi na fani zilizomo katika ushairi huo wa Shaaban Robert.

1.4 Malengo ya Utafiti

1.4.1 Lengo kuu la Utafiti

Utafiti huu una lengo la kuchunguza dhamira ya mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert.

1.4.2 Madhumuni Maalumu ya Utafiti

Utafiti huu una madhumuni maalumu yafuatayo:-

i) Kuainisha dhamira za mapenzi katika *Mapenzi Bora.*

ii) Kuchambua dhamira za mapenzi zilizojitokeza katika *Mapenzi Bora.*

iii) Kuchunguza vipengele vya fani kwa upande wa lugha na muundo vilivyojitokeza katika *Mapenzi Bora.*

1.4.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unakusudia kujibu maswali yafuatayo:-

i) Ni dhamira zipi za mapenzi zinazojitokeza katika *Mapenzi Bora?*

ii) Ni dhamira gani za aina ya mapenzi zilizojitokeza na kuchambuliwa katika kitabu cha *Mapenzi Bora?*

iii) Ni vipengele gani vya fani vilivyojitokeza katika kitabu cha *Mapenzi* Bora*?*

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utatumika kama rejeleo kwa wataalamu wote wanaojishughulisha na masuala ya fasihi ya Kiswahili hususani Ushairi wa Kiswahili.

Wanafunzi wa masuala ya fasihi watatumia utafiti huu katika kujifunza namna ushairi ulivyo na kujua dhamira za mapenzi na fani katika *Mapenzi Bora.*

Kwa watafiti wa masuala ya fasihi, watauona utafiti huu kama sehemu muhimu ya wao kupata maeneo zaidi ya kufanyia utafiti katika kazi za Shaaban Robert. Shaaban Robert amefanya kazi nyingi ambazo zinahitaji kufanyiwa uhakiki na uchambuzi zaidi. Hivyo, kupitia utafiti huu, watafiti wanaweza kuyaona maeneo mbalimbali ya kushughulikia.

Wahadhiri wa vyuo vikuu pia watafaidika katika utafiti huu kama rejeleo muhimu katika kuandaa vitabu, makala na insha kwa ajili ya wanafunzi wao. Hii itawafanya

wapate maelezo tosha juu ya dhamira ya mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora*.

1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza dhamira ya mapenzi na fani ambavyo ni katika upande wa lugha na muundo katika kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert.

Shaaban Robert katika vitabu vyake vingi vya mashairi ameelezea mapenzi lakini katika kitabu chake hiki cha *Mapenzi Bora*, mada hii ya mapenzi inajitokeza tofauti zaidi. Hii pia inaleta utofauti wake na watunzi wengine, kwani yeye ni mtunzi pekee ambaye ameweza kuandika beti takriban 700 , ambazo zote zimeelezea mapenzi.

1.7 Vikwazo vya Utafiti

Mtafiti alikumbana na vikwazo kadhaa. Kwanza kubwa ni muda wa kuingia maktabani kwa sababu alikuwa na muda finyu wa kutoka kazini. Pili ni kutokana na kuwa na mtoto mdogo ambaye muda mwingine alikuwa anashindwa kufanya kazi zake za utafiti.

1.8 Utatuzi wa Vikwazo

Mara nyingi mtafiti alikuwa anatumia muda wa jioni, Jumamosi na Jumapili kuingia maktabani. Alisubiri mtoto akuwe kidogo ili awe makini katika utafiti wake ,ingawa hali hii ilimfanya achelewe kumaliza utafiti wake.

1.9 Wasifu wa Shaaban Robert

Shaaban Robert ndiye mtunzi wa kitabu cha *Mapenzi Bora* ambacho kinachunguzwa katika utafiti huu wa swali "Kuchunguza dhamira ya Mapenzi katika kitabu cha *Mapenzi Bora*".

Nguli huyu alizaliwa tarehe 1 mwezi wa 1 mwaka 1909, huko Vibambani Tanga. Alikuwa ni mtoto pekee wa Bi Mwanamwema kwa Bwana Robert (au Ufukwe Selemani bin Jumaa). Shaaban Robert alianza shule mwaka 1922 na kumaliza 1926 katika shule ya Kichwele ambayo kwasasa inafahamika katika Uhuru Mchanganyiko. Alipenda sana kusoma na kujiendeleza kielimu lakini jitihada zake hazikuzaa matunda kwa haraka kwasababu ziliporwa na wakoloni kwa lengo la kumtumia kama chombo cha kutawalia. Hata hivyo mwaka 1932 aliendelea na masomo yake kwa njia ya posta ambako mwaka 1934 alitunukiwa Diploma ya Fasihi. Mwaka 1936-37 alitunukiwa cheti cha English level. Ni dhahiri kuwa Shaaban Robert alikuwa ni mtu mwenye bidii kubwa katika kujiendeleza kielimu na kama si wakoloni angalifika katika ngazi za juu zaidi.

Ilipofika mwaka 1926 alianza kazi katika idara ya Forodha Tanga. Hapo alidumu kwa miaka takriban 18. Mwaka 1946 alirudishwa Tanga na kuwa Afisa Ardhi wa jimbo la Tanga. Aidha barua zake pia zinaonesha aliwahi kufanya kazi katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Dar es Salaam na Kisiju, Pangani, Moshi, Longido, Mpwapwa n.k. Kutokana na utendaji mzuri, Shaaban Robert alipanda cheo kutoka katika ngazi ya karani Daraja la pili mwaka 1944. Alipata pia kuwa mjumbe wa asasi mbalimbali zilizohusu lugha, taaluma na utawala, zikiwemo Kamati ya Kiswahili ya

Afrika Mashariki (Kuanzia mwaka 1953), Bodi ya Lugha ya Tanganyika, Chama Cha Majadiliano cha Tanga na Halmashauri ya mji wa Tanga. Vilevile alipata kutunukiwa tunzo ya uandishi ya *Margaret Wrong Prize*, tunzo ya Mjumbe wa Himaya ya Kiingereza, na tunzo ya Mwandishi Bora ya Wizara inayosimamia Utamaduni nchini Tanzania (mwaka 1987). Shaaban Robert alifariki tarehe 20.6,1962 na kuzikwa huko Vibambani tarehe 21.6,1962 (Robert, 2008).

1.10 Hitimisho

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano, ambazo zimeeleza masuala mbalimbali yaliyosaidi kukamilika kwa tasnifu hii. Sura ya kwanza imewasilisha utangulizi kwa ujumla, ambao utangulizi huo una vipengele kama usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wa vikwazo. Sura ya pili imewasilisha utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu inahusu mbinu na zana za utafiti, sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti na sura ya tano na ya mwisho inahusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

SURA YA PILI

2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika utafiti huu tumetalii kazi tangulizi, ambazo zimetafiti na kuhakiki kazi mbalimbali za Shaaban Robert. Kwa hakika kazi nyingi za uhakiki kuhusu Shaaban Robert zimefanywa. Miongoni mwa wahakiki na wachambuzi wa kazi hizo ni Kezilahabi (1976a), Kezilahabi (1983) ,Njogu na Chimerah (1999), Momanyi (2001), Twaib (2009) na Chuachua (2011) .Lakini pamoja na tafiti zao hizo hawakulenga kuchunguza dhamira ya mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert. Watafiti hao walikuwa na malengo tofauti tofauti na utafiti huu.

Momanyi (2001) , aliandika makala juu ya nafasi ya mwanamke katika ushairi wa Shaaban Robert. Katika makala yake hiyo alionesha kuwa Shaaban Robert anamsawiri mwanamke katika hali mbili. Kwamba hali ya kwanza mwanamke kama ni mlezi katika jamii, mkarimu, mpole, mnyenyekevu na kadhalika. Hali ya pili mwanamke kama kiumbe duni katika jamii. Mawazo haya ni kweli yapo katika jamii zetu lakini bado utafiti wake haujagusa lengo la utafiti huu.

Kezilahabi (196b) aliandika tasnifu yake ya Uzamili juu ya “Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya”. Pamoja na kuwa kazi hii ilihusu riwaya lakini pia alitumia kazi moja ya kishairi ya *Mapenzi Bora* sambamba na riwaya za Shaaban Robert lakini bado haijalenga dhumuni la utafiti huu. Zaidi katika tafiti hii ameelezea kuwa

Shaaban Robert amemuona mama kuwa ni kiumbe mvumilivu na mpole, lakini masuala ya mapenzi kama lilivyo lengo la utafiti huu hajaligusia hata kidogo.Kwa hiyo utafiti huo bado haujagusia masuala ya mapenzi lakini itasaidia katika kupata dondoo mbalimbali.

Sengo (1975) aliandika juu ya mada isemayo, Shaaban Robert: *Uhakiki wa Maandishi yake.* Katika uhakiki huo, Shaaban Robert anaelezwa kuwa alikuwa mtu ambaye alijali sana ubinaadamu katika jamii. Alipenda kuona kuwa kila mtu anapata heshima yake, haki zake na kutendeana mema kati ya wanaadamu na jamii. Mawazo hayo yalikuja katika kipindi ambacho Tanganyika ilikuwa imetawaliwa na wakoloni ambao hawakujali haki za watanganyika. Maelezo hayo ya Sengo (1975) yana umuhimu sana katika utafiti huu kwasababu yanamwelezea Shaaban Robert kama mtetezi wa haki katika jamii, kutokana na hili inathibitika kwamba, Shaaban Robert amekusudia kuwepo kwa mapenzi, kwani kama mapenzi hakuna basi haki pia haitozingatiwa.

Maganga (1971) anaelezea kwamba, Shaaban Robert ni mtu ambaye alikuwa na mawazo ya kimapinduzi ambayo yalilenga kumkomboa kila Mtanzania hususani mwanamke kutokana na mateso mbalimbali yanayomkumba katika jamii. Shaaban Robert anaonesha kuwa mwanamke ndiye anayebeba ujauzito wa mtoto wa miezi tisa na baadae kumlea mtoto huyo mpaka kuweza kujitegemea yeye mwenyewe. Katika mazingira mengine mwanamke huachiwa majukumu ya kulea watoto peke yake huku mwanamume akiishia katika ulevi na anasa nyingine za kidunia. Shaaban aliipinga hali hii na kuitaka jamii kumhurumia mama na kumpatia msaada wowote

atakao uhitaji ili aishi maisha mazuri. Mawazo hayo ya Maganga (1971) hapo juu yanaonesha kwamba , Shaaban Robert amempatia mwanamke nafasi ya ulezi na huruma katika jamii huku akiona mwanaume kutokuwa na sifa hizo.

Mawazo hayo yamesaidia sana katika tafiti hii japo lengo lake kuu halikuwa kuonesha mapenzi bali linasisitiza kuwa jamii kuwa na mapenzi na wanawake kwani wao ni viumbe wanayoibeba jamii kwa hali ya juu kabisa, mfano mzuri katika malezi. Hivyo basi, kutokana na baadhi ya tafiti hizo, mtafiti ameona kuna haja ya kuziba pengo lililoachwa juu ya dhamira ya mapenzi na fani katika kazi za Shaaban Robert hasa kwa kutumia kitabu cha *Mapenzi Bora.*

2.2 Pengo la Kimaarifa

Baada ya kutalii kazi tofauti zilizopita ambazo zimeelezea kazi za Shaaban Robert, utafiti huu umebaini kuwa tafiti nyingi zilizofanywa zimejikita katika kuchunguza masuala mbalimbali yanayoibuka katika jamii. Mpaka sasa hakuna utafiti wa kina uliyofanywa ambao unachunguza kwa kina dhamira ya mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora*. Pengo hili ndilo ambalo utafiti huu ulikusudia kuliziba.

2.3 Dhana ya Ushairi

Ushairi ni utanzu ambao una historia ndefu katika fasihi ya Kiswahili. Ingawa bado hayajapatikana makubaliano kuhusu utungo wa kwanza wa kishairi uliandikwa lini, wataalamu wanakubaliana kuwa utanzu huu una historia ndefu. Wapo wataalamu wanaosema kuwa utungo wa kwanza uliyotungwa ni *utendi wa Mwanayanga* unaodaiwa ulitungwa na Fumo Liyongo katika mwaka wa 1517 (Wamitila, 2008).

Nao Warren na Wellek (1985) wanasema kuwa ushairi ni utungo utumiao mfumo maalumu wa maneno katika kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Ujumbe unaweza kuwa wa furaha, huzuni au masimulizi ya hadithi fulani.

Krappert (1974) anaona ushairi kama taaluma iliyokamilika katika kueleza ukweli wa maisha katika jamii husika.

Pamoja na maelezo kwamba, ushairi ni taaluma, ushairi ni utungo wa mwanzo kabisa kuliko tungo nyingine zote za fasihi simulizi, Sanka (1994) anaongeza kwamba, ushairi umekuwa chombo muhimu katika kuongeza historia, falsafa na utamaduni wa jamii. Anaendelea kusema kuwa, ushairi ni zao la jamii husika na hivyo huwa na sifa maalumu kulingana na muktadha lengwa kwa jamii inayohusika.

Maelezo hayo bila shaka yanatoa mwanga kwamba, kwa vile ushairi ndiyo utanzu wa mwanzo kabisa kupatwa kutungwa na wanadamu, hivyo twaweza kusema ushairi ndiyo utanzu wa mwanzo uliyoweza kuchambua na kuelezea masuala ya mapenzi katika jamii. Kutokana na uelewa huu kuhusu ushairi, unampatia hamu mtafiti wa kutafiti ushairi wa Shaaban Robert wa *Mapenzi Bora* ili kubaini dhamira ya mapenzi na fani.

2.4 Dhana ya Dhamira

Dhamira ni ile jumla ya maana anayoivumbua msomaji katika usomaji wake (Wamitila, 2002). Dhamira hutumika kurejelea mada ya kazi fulani au ujumbe au lengo la kazi hiyo. Kwa kawaida kuna aina mbili za dhamira, dhamira kuu na dhamira ndogondogo. Kutokana na maneno ya Wamitilla (2002), kwa kila ya kazi ya

fasihi lazima kuwe na dhamira ambayo mwandishi ameikusudia ili hadhira ipate kufaidika kwa kupata ujumbe.

2.5 Dhana ya Fani

Kwa maelezo ya Wamitila (2003), fani inaelezwa kuwa ni dhana inayotumiwa kuelezea muundo au mpangilio wa dhana fulani ya kifasihi. Aghalabu wahakiki hupenda kutofautisha kati ya fani na maudhui, lakini ni muhimu sana kukumbuka kuwa dhana mbili hizi hatuwezi kizitenganisha. Mawazo haya hayatofautiani na mawazo ya Senkoro (1982) kuhusu fani. Fani katika tasnifu hii inachukuliwa kuwa ni umbo la nje ya kazi ya fasihi, na ni vipengele vinavyotumika kuwasilisha maudhui ya kazi husika ya kifasihi.

Katika kitabu cha *Mapenzi Bora* kilichotumika katika utafiti huu, kuna vipengele vingi vya fani vilivyoweza kujenga dhamira na hatimaye kuifikia jamii. Moja ya madhumuni mahsusi katika utafiti huu ilikuwa ni kubainisha vipengele vya kifani. Vipengele hivyo vya fani kwa upande lugha ambavyo vimeangalia tamathali za usemi na muundo wa shairi.

2.6 Tamathali za Usemi

Msokile (1993) anaeleza kwamba, tamathali za usemi ni maneno, nahau au semi ambazo hutumiwa na waandishi wa fasihi ili kutia nguvu na msisitizo katika maana, mtindo na pengine sauti katika maandishi hayo.

Tamathali za usemi pia zinatumiwa katika kupamba kazi ya sanaa ya kifasihi kwa kuongeza utamu wa lugha. Hivyo katika utafiti huu, mtafiti amechunguza vipengele

vya lugha na muundo ambavyo vimetumika katika kitabu cha Shaaban Robert cha *Mapenzi Bora*.

2.7.1 Tashibiha

Ni usemi wa kimlinganisho utumiao maneno kama; mithili ya, kama kwamba. Kwa mfano; Mrefu kama jini, mweusi kama mkaa, mwembamba kama chelewa. Mifano hii tashibiha kwasababu inalinganisha vitu vyenye umbo na sifa tofauti kwa kutumia maneno yaliyotajwa katika sehemu hii.

2.7.2 Takriri

Njogu na Chimerah (2014) wamefasili kuwa takriri ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa na watunzi wa ushairi kurudia rudia baadhi ya silabi na maneno katika kazi zao ili kuleta msisitizo kwa jambo ambalo wanadhani ni muhimu kwa wasomaji kulinasa mara moja.

Senkoro (1988) anasema, takriri ni kama chombo kinachotumika katika kumkumbusha msomaji kile kilichosomwa katika ubeti uliyotangulia na kuhusianisha na kile anachosoma.

2.7.3 Tashihisi

Senkoro (1988) anafasili kuwa tamathali ya usemi ambayo wakati mwingine huitwa tamathali ya binaadamu. Katika tashihisi kuna vitu visivyo na sifa walizonazo watu hupewa sifa hizo viumbe vingine au vitu vingine. Mfano; Miti ilishangilia kwa furaha. Kwa kawaida miti haiwezi kushangilia, kwa hiyo sifa hiyo ya binaadamu

imepewa miti ili kuonyesha tashihisi kwa kuipamba lugha katika kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe

2.7.4 Sitiari

Hii ni tamathali ya usemi ambayo kwa kawaida inalinganisha matendo, kitu au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti. Ulinganisho huu unazingatia tabia au sifa inayopatikana au zinazopatikana katika vitu viwili ,lakini sifa hizo haziwi wazi kati ya kitu na kitu. Mfano;

i) Maisha ni moshi
ii) Amina tausi
iii) Ana mwendo wa kobe

Kutokana na mifano hiyo juu, maisha yamefananishwa na moshi kwasababu moshi unapotokea hukaa kwa muda mfupi sana kisha utoweka kabisa, halikadhalika na maisha yamefanishwa na moshi kwasababu ni mafupi na yenye kupita kama moshi. Mfano wa pili Amina amefananishwa na tausi kutokana na uzuri wake, na mfano wa tatu mwendo wa kobe kwasababu anatembea taratibu, hiyo yote ni mifano ya sitiari ambayo kwa kawaida inatumika bila ya kuangalia viunganishi.

Kwa ufupi sitiari ni tamathali ya usemi inayolinganisha vitu bila ya kutumia viunganishi kama vile mithili ya, mfano wa, sawa na, na kadhalika (Omary, 2010;2011)

2.7.5 Taswira

Taswira ni picha anayoipata msomaji pindi asomapo kazi husika. Taswira hupatikana

na ishara, tashibiha ,sitiari na pengine uhalisia mazingaombwe (Senkoro 1982; 2006) .Kwa mfano usomapo riwaya ya Nagona (1990) unakutana na mambo mengi ya ajabu ajabu kama vile maiti anaongea, mtoto anaongea akiwa tumboni. Uajabu ajabu huo hutoa picha au taswira ya jambo fulani katika jamii tuishio. Maana hizo ambazo huweza kuibuliwa na mwitikio wa msomaji ndiyo inaweza kuwa picha au taswira inayozungumziwa katika utafiti huu.

2.8 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia ni muongozo unaotoa maelekezo juu ya namna au jambo fulani linalopaswa kufanywa au kufanyika ili kutoa matokeo yasiyoweza kutiliwa shaka ya kitaaluma kwamba ni sahihi au si sahihi (Kothari, 2008). Katika utafiti huu nadharia ya Fani na Fasihi na Jamii zimetumika katika kuchambua data za utafiti.

2.8.1 Nadharia ya Fani

Kupitia http://www.slideshare.net/mariaraja 232/formalism-literary-theory inaelezwa kwamba nadharia hii inajihusisha kwa kiasi kikubwa na mbinu mbalimbali za kifani katika kazi ya fasihi. Inaelezwa kuwa fani katika fasihi ni sehemu muhimu sana kwani ndiyo inayojenga madhumini ya kazi husika. Hivyo, ni vigumu sana kutenganisha fani na maudhui. Nadharia hii ilianzishwa huko Marekani mwishoni mwa vita vya pili vya dunia, ambapo waasisi wake ni pamoja na I. A. Richard, John. Crowe pamoja na T. S. Eliot. Barry, (1995).

Kwa upande wa Sengo (1990) amejaribu kufafanua zaidi na kueleza kuwa kuna masuala kadhaa yanayozingatiwa katika nadharia hii. Miongoni mwa masuala hayo

ni pamoja na suala la matumizi ya lugha. Anaeleza kwamba, nadharia hii hujiegemeza zaidi na suala la kupambika kwa fani ya usemaji na uhodari wa kutumia lugha. Semi ni moja kati ya vipengele vya fasihi ambavyo huipamba lugha. Semi hizi hujitokeza katika kazi ya fasihi zikiwa zimefumbwa kwa kutumia picha, ishara na tamathali mbali mbali. Hivyo, mtafiti anaona kuna haja na umuhimu wa kuitumia nadharia hii kwasababu itamuongoza kuwa makini katika matumizi ya lugha yaliyojitokeza katika kitabu cha *Mapenzi Bora* kwa mada ya kuchunguza dhamira ya mapenzi na fani.

2.8.2 Nadharia ya Fasihi na Jamii

Uhusiano wa fasihi na jamii umethibitishwa kwa kupitia fasili nyingi za fasihi, hivyo uhusiano wa dhana hizi mbili hauwezi kupuuzwa. Miongoni mwa wataalamu wanaoiunga mkono dhana hii ni pamoja na Escarpit (1974:4) anasema kwamba: “Fasihi ni lazima ichukuliwe kama ilivyo na uhusiano usiyotatanika na maisha ya jamii”.Mfano mzuri wa mahusiano hayo yanaonekana katika mabadiliko ya fasihi kutoka simulizi hadi andishi, jambo ambalo lilisababishwa na mabadiliko ya jamii yenyewe kutoka katika masimulizi hadi kufikia katika hatua ya kusoma na kuandika. Hivyo basi, jukumu la fasihi ni la kijamii na wala si mtu binafsi.

Werren na Wellek (1949) wanaiunga mkono kauli hii na kufafanua kama ifuatavyo, “Uhusiano kati ya fasihi na jamii hujadiliwa kwa kuanza na kauli aliyeitoa De Benald kwamba, fasihi ni kielelezo cha jamii”

Kutokana na maelezo hayo, tunaona fasihi inakuwa na kubadilika kutokana na jamii husika. Katika jamii kuna mambo mengi kama vile usaliti, dhulma, chuki, na

kadhalika. Mambo yote hayo fasihi inaviakisi na kufikisha ujumbe kwa jamii. Halikadhalika suala la mapenzi pia ni la kijamii ambalo linaelezwa kila kukicha katika kazi za fasihi na jinsi jamii inavyoyachukulia mapenzi.

Hivyo basi, mtafiti ameamuwa kuchagua nadharia hii ambayo itaweza kuchumbua dhamira za mapenzi zilizojitokeza katika utafiti huu wa mada inayosema kuchunguza dhamira ya mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert ambayo anaamini itakuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu, kwasababu itaweza kusaidia kufafanua suala la mapenzi ambayo yapo katika jamii na imani za watu zinabadilika kila kukicha na kila fasihi inavyokuwa. Mapenzi waliyokuwa nayo watu wa kabla yetu ni tofauti na mapenzi tuliyonayo sasa.

2.9 Hitimisho

Utalii wa kazi tangulizi uliyofanywa katika sura hii unaonesha kuwa, hakuna mtafiti aliyefanya utafiti wa kina kuchunguza dhamira ya mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert.Katika sura hii pia tumewasilisha nadharia mbili ambazo ni nadharia za Fani na nadharia ya Fasihi na Jamii. Na kueleza namna zilivyotumika katika uchambuzi wa data. Sura inayofuata inahusu mbinu za utafiti.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Utafiti ni sayansi ambayo hufanywa kwa kuongozwa na taratibu maalumu ambazo mwisho wa siku, zikifuatwa vizuri, hutoa matokeo stahiki pasipo upendeleo wowote, (Babbie, 1999). Taratibu ambazo zinatakiwa kufuatwa katika kufanya utafiti zinaitwa mbinu za utafiti. Hivyo, sura hii inawasilisha mbinu zitakazotumika katika uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafi huu. Mbinu hizo ni mbinu za maktabani na usomaji makini.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu wa kuchunguza dhamira za mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora* umefanyika Dar es salaam ndani ya maktaba ya Chuo Kikuu Huria na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mtafiti alivutiwa kufanyia utafiti wake katika eneo hili kwa sababu ni rahisi kupata data zinazohusu mashairi ya Shaaban Robert, hasa ukizingatia eneo hili, Dar es Salaam, lina vyuo, maktaba na Taasisi zinazojishughulisha na ufundishaji, utafiti na ushauri wa fasihi ya Kiswahili kwa kiwango cha juu.

3.3 Watafitiwa

Watafitiwa hurejelea idadi ya watu na vitu vyote ambavyo mtafiti amevitafuta na kuvitumia ili kukamilisha utafiti wake, kwa upande mwingine watafitiwa huweza kutafsiriwa kama mkusanyiko wa watu au vitu kutokana na mazingira husika.

Watafitiwa katika utafiti huu ni kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert.

3.4 Sampuli na Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Ni sehemu ya watafitiwa ambayo huteuliwa ili kuwa wawakilishi ambao hufanywa kuwa kundi lengwa la utafiti (Kombo na Tromph, 2006). Sampuli lengwa na nasibu ndizo zilozotumika na kufanikisha ukusanyaji wa data.

3.4.1 Kundi Lengwa (Sampuli na Usampulishaji)

Sampuli lengwa ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huiteua akiamini kwamba, itampatia data zitakazomwezesha kukamilisha malengo ya utafiti wake (New Man, 2006:22).Usampulishaji ni kitendo cha kuteua washiriki katika kundi kubwa la watafitiwa ili kupata idadi ndogo ya watafitiwa watakaotumiwa katika kutoa data za utafiti. Utafiti huu umetumia aina mbili za sampuli nambazo ni sampuli lengwa na sampuli nasibu.

Kutokana na utafiti huu, hapa kundi lengwa ni kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert.Mtafiti ameteua kitabu hiki kwasababu anaamini ndicho kitachompatia majibu ya maswali yake ya utafiti.

3.4.2 Sampuli Nasibu

Ni ile ambayo hutoa fursa sawa kwa watafitiwa wote kuchaguliwa ili kutoa data za utafiti kama ilivyokusudiwa na mtafiti (Babbie,1999). Sampuli nasibu iliyotumika katika kukusanya data kutoka katika utenzi ambao upo katika kitabu cha *Mapenzi Bora.* Pale mtafiti alipobaini beti na vipande vya shairi na kuweza kuibua dhamira za

mapenzi au fani katika shajara kwa ajili ya uchambuzi. Hivyo basi, sampuli zote yaani lengwa na nasibu zimeweza kusaidia kukusanya taarifa zilizowezesha kutimiza malengo ya utafiti.

3.5 Aina za Data Zilizokusanywa

Kuna aina mbili za vyanzo vya data za utafiti katika utafiti wowote ule wa kitaaluma. Aina hizo ni data za msingi na data za upili.

3.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile data zinazotumika kurejelea data zinazokusanywa kwa mara ya kwanza kabisa katika utafiti husika na hazijawahi kukusanywa na mtu mwingine kwa ajili ya utafiti kama huu anaofanya mtu huyo kwa wakati huu (Kothari, 2008).

Data za msingi zinaweza kukusanywa maskanini kwa mtafiti kwa njia ya usaili, mahojiano hata ushuhudiaji na ushiriki kutokana na mada. Lakini kutokana na mada ya utafiti huu, usomaji makini katika kitabu kilichoteuliwa, zimewezwa kukusanywa data.

3.5.2 Data za Upili

Data za upili ni zile zilizokwisha kukusanywa na watafiti wengine na kuandikwa au kuwasilishwa katika vitabu, tasnifu , majarida na hata tovuti mbalimbali. Data hizi hukusanywa kwa lengo la kujazilizia data za msingi ambazo zinakusanywa kutoka maskanini. Hivyo basi, mtafiti ataweza kupata data hizo kwa kusoma tasnifu, vitabu, makala na tovuti mbalimbali kutokana na mada. Katika utafiti huu, data za upili zilikusanywa kutoka katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data

Mbinu ni namna mtu anavyoweka mikakati ya kufanikisha jambo alilolikusudia. Kothari (2008), mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa wakati wa kufanya utafiti.

Data zimekusanywa kwa utaratibu maalumu uliyobuniwa na mtafiti. Mtafiti alikusanya data kwa kutumia mbinu mbili ambazo ni mbinu za maktabani na mbinu za usomaji makini.

3.6.1 Mbinu ya Usomaji Makini

Usomaji makini ni mbinu ya kukusanya data za msingi. Mtafiti anatakiwa kusoma kwa makini matini husika akidondoa na kunukuu data zinazojibu maswali yake ya utafiti katika daftari maalumu alililoliandaa, Kothari (2008).

3.6.2 Mbinu za Maktabani

Mbinu ya usomaji wa maktabani uhusisha kutafuta data kwa kusoma vitabu mbalimbali, majarida, vitabu teule, tasnifu na vitabu vya ziada kulingana na malengo ya utafiti ili kupata data zitakazomkidhi mtafiti. Mbinu hii ilitumika katika utafiti huu ambapo mtafiti alisoma kitabu teule, majarida, tasnifu na vitabu vya ziada ambavyo vilimwezesha kupata data na taarifa muhimu za utafiti huu.

3.7 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vilivyotumika kukusanyia data katika utafiti huu ni matini ya kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert, daftari dogo kwa ajili ya kuandika mambo

muhimu wakati wa kusoma kitabu na majarida, ngamizi ambayo ilimsaidia mtafiti katika kuangalia tovuti na wavuti pamoja na kuhifadhia taarifa muhimu. Peni pia ilitumika katika kuandikia nukuu na data mbalimbali zilizokusanywa.

3.8 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data katika utafiti huu ulifanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi inayojulikana kama mbinu ya mkabala wa kimaelezo (Babbie, 1999). Kothari (2008) anasema kwamba, mkabala wa kimaelezo hutoa fursa kwa mtafiti kuziainisha data zake katika makundi mbalimbali kulingana na mada yake ya utafiti na kisha kuzipanga kwa namna ambayo itakuwa rahisi kwake kufanya uchambuzi wa data zake.

Hivyo basi, mbinu hii itahusu utolewaji wa kina juu ya data zilizokusanywa na mtafiti kwa namna ambayo itawezesha kujibu maswali ya utafiti.

Uchambuzi wa data umezingatia malengo ya utafiti ambayo yaliyowekwa na kuainisha dhamira ya mapenzi pamoja na vipengele vya fani vinavyojitokeza katika kitabu cha *Mapenzi Bora.*

3.9 Hitimisho

Sura hii kimsingi imefafanua mambo kadhaa ambayo ni msingi kujadiliwa. Baadhi ya mambo hayo ni mbinu zilizomuongoza mtafiti kupata data, eneo la utafiti, vifaa vya utafiti na njia iliyotumika kuchambua data. Sura inayofuata itahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa kwa ajili ya utafiti huu.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Kutokana na utafiti wetu, hii ni sura mama. Sura hii ndiyo inayowasilisha mambo muhimu ambayo yanaweza kutimizwa kwa malengo ya utafiti. Young (1984) anaeleza kuwa, utafiti hauwezi kukamilika mpaka pale matokeo ya utafiti huo yanapowasilishwa kwa namna inayokubalika kitaaluma. Hivyo, uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti huu umefanywa kwa kurejelea madhumuni mahususi ambayo jumla yake ni matatu. Madhumuni mahsusi ya kwanza yalikuwa kuainisha dhamira za mapenzi katika kitabu cha *Mapenzi Bora*. Madhumuni mahsusi ya pili yalihusu kuchambua dhamira za mapenzi katika kitabu cha *Mapenzi Bora*. Madhumuni ya tatu na ya mwisho yalikuwa kuchunguza vipengele vya fani vilivyojitokeza katika kitabu cha *Mapenzi Bora*. Baada ya utangulizi huu, ni vema sasa kutazama madhumuni mahsusi ya kwanza yalivyotizamwa katika utafiti huu.

4.2 Kuainisha Dhamira za Mapenzi Katika Kitabu cha Mapenzi Bora

Katika kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert, dhamira yake kuu ni juu mapenzi. Pamoja na kuwa na dhamira hii kuu ya mapenzi ambayo ndiyo itakayoangaliwa katika utafiti huu lakini pia zitaainishwa dhamira za mapenzi kutokana na kitabu hiki cha *Mapenzi Bora* kama mtafiti alivyoweza kupata data zake na kuziainisha katika makundi saba:

i) Mapenzi ya Mungu

ii) Mapenzi ya Mitume

iii) Mapenzi ya Sisi kwa Sisi

iv) Mapenzi yasiyoangalia Kabila, Taifa wala Rangi

v) Mapenzi ya Majirani na Marafiki

vi) Mapenzi ya Kudumu

vii) Mapenzi ya Nchi

4.3 Kuchambua Dhamira za Mapenzi Katika Kitabu cha Mapenzi Bora

Hili ni dhumuni mahsusi la pili katika utafiti huu ambalo linahusu kuchambua dhamira za mapenzi katika kitabu cha *Mapenzi Bora* cha Shaaban Robert, tukirejea sura ya pili tunaona Wamitila (2002), ameeleza maana ya dhamira kwa kusema "Dhamira ni ile jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo, na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake". Kutokana na maelezo hayo, dhamira za mapenzi zilizoainishwa zitaanza kuchambuliwa kama ifuatavyo:-

4.3.1 Mapenzi ya Mungu

Mtunzi Shaaban Robert, amesisitiza juu ya mapenzi kwa Mwenyezi Mungu, kwani mapenzi yake ni mapenzi ambayo hayana mfano, ni mapenzi yasiyo na chuki, inda, utabaka wala udanganyifu. Lau kama mapenzi ya Mwenyezi Mungu yangekuwa na mapungufu hayo basi hata riziki na neema zote alizotujaalia waja wake tusingezipata. Katika baadhi ya beti zake juu ya mapenzi ya Allah anasema;

122 Tusihini walimwengu
Mapenzi tumpe Mungu
Naye atatupa fungu
Katika wake wenezi.

Sehemu nyingine anasema tumpende Mwenyezi Mungu, kwasababu punje ya pendo katika moyo wa mwanaadamu, ni kama jua katika dunia. Kwa msingi huu inaonesha

wazi,mapenzi yana athari kubwa katika moyo wa mwanadamu. Ili tupate thamani ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu, hatuna budi kuzidisha mapenzi kwake.

260 Punje ya pendo moyoni
Kama jua duniani
Na kuzidisha thamani
Yake mtu kwa Mwenyezi.

4.3.2 Mapenzi ya Mitume

Mwandishi Shaaban Robert, katika kitabu chake ametutaka tuige na tufuate nyayo za mitume. Katika imani zote za dini tunaamini mitume ni watu waliyotumwa na Mwenyezi Munyezi Mungu ili waje kutuongoza katika kufanya mema na kutukataza mabaya. Kutokana na cheo chao walichopewa na Mwenyezi Mungu walikuwa na mapenzi ya kweli yenye huruma na imani. Ndiyo sababu mtunzi ametusisitizia juu ya mapenzi ya mitume kama ifuatavyo:

121 Ni mapenzi ya mitume
Yaliyo shinda kinyume
Na sisi tufanye shime
Kuandama nyayo hizi.

Tukiangalia leo katika jamii, huruma na mapenzi ya kweli hakuna. Mke anashindwa kumvumilia mume wake, na mume pia anashindwa kumvumilia mke wake, mwalimu anashindwa kumvumilia mwanafunzi wake na mwanafunzi pia anashindwa kumvumilia mwalimu wake, hayo si mapenzi ya mitume yalivyokuwa. Inabidi jamii ifuate nyayo za mitume katika kuonyesha mapenzi. Mitume walikuwa na mapenzi ya kweli yenye uvumilivu ndani yake.

4.3.3 Mapenzi ya Sisi kwa Sisi

Shaaban Robert, katika ubeti mwingine ameelezea jinsi ya umuhimu wa kupendana sisi kwa sisi. Tukipendana basi chuki zitatoweka, amani itakuwepo na maendeleo

yatapatikana. Kwasababu kwenye chuki na uhasama kamwe hakuwezi kuwa na maendeleo. Wanaadamu yatupasa tupendane, tuelewane, tuhurumiane na tusikilizane ili tupate baraka toka kwa Mwenyezi Mungu. Shaaban Robert anasema:-

123 Tupendane na wenyewe
Tofauti tuondowe
Amani itushukie
Mapenzi tufanye ngazi.

4.3.4 Mapenzi Yasiyoangalia, Kabila, Taifa wala Rangi

Shaaban Robert katika kitabu chake anasema, mapenzi ya dhati yaliyo bora hayaangalii, kabila, taifa wala rangi. Kama katika jamii kungekuwa na mapenzi ya kweli basi matatizo mengi ya chuki na husda yasingetokea. Na kwasababu kazi za fasihi zina akisi jamii ilivyo, ndiyo maana Shaaban Robert ameliona hilo na kulifikisha kwa jamii. Wanaadamu hatuna haja ya kubaguana kwa kuangalia kabila la mtu, rangi yake au taifa lake. Shaaban Robert, anakemea kabisa la kubaguana kwa kuangalia kabila la mtu ,taifa lake au rangi yake. Hili litasababisha watu washindwe kufanya kazi pamoja, kuowana, kusaidiana na hata kuzikana. Kwa vyoyote vile sehemu yenye ubaguzi hata maendeleo yatakosekana, amani itatoweka na chuki na maovu yatatawala. Mshairi anasema:

147 Mapenzi wanayo mengi
Wanadamu kila rangi
Lakini hawayaungi
Kwa sera ya ubaguzi.

148 Wa Ulaya wamba bora
Asia wamba tohara
Marekani masogora
Haya yao si mapenzi.

4.3.5 Mapenzi ya Kudumu

Mtafiti wa utafiti huu, katika kitabu cha Shaaban Robert ameweza kugundua aina

nyingine ya mapenzi ambayo ni mapenzi ya kudumu. Mshairi ameelezea hayo kwasababu wanadamu wengi katika jamii zetu wamekuwa na mapenzi kinafiki, mapenzi ya kutojuana wakati wa shida, na inapotokea shida yoyote kama misiba, maradhi na misukosuko basi utakuta mtu anakimbia na hii yote ni kutokana na kukosekana mapenzi ya maki yaani mapenzi ya kweli na yenye nguvu. Mapenzi haya ya kudumu si mapenzi ya ndoa tu bali hata mapenzi kati ya rafiki na rafiki, jirani kwa jirani au nchi kwa nchi. Shaaban Robert nasema kwamba;

116 Mapenzi niyanenayo
Ya saburi na makao
Milele katika moyo
Si mapenzi makimbizi.

120. Siyo yapigayo mbio
Wakati wa majilio
Ya msiba na kilio
Ukabaki bila mwenzi.

4.3.6 Mapenzi ya Majirani na Marafiki

Shaaban Robert, amesisitiza mapenzi pia kwa marafiki na majirani kwa kusema:

139 Ni himaya kwenye dhiki
Kwa ndugu na marafiki
Hasa mapenzi ya maki
Ambayo si makimbizi.

140 Ni johari ya thamani
Kwa kuunga majirani
Kama watoto nyumbani
Na nasaba ya uzazi.

Mtunzi ameweza kuonyesha haja ya kuwepo mapenzi ya kweli kwa majirani na marafiki, kwani jirani na marafiki ni ndugu wa karibu sana. Wao wanapaswa kuheshimiwa, kuthaminiwa na kupewa mapenzi makubwa. Na wana uwezo wa kutoa msaada mkubwa pindi tunapopatwa na jambo lolote. Hivyo basi, kuna haja ya kuwathamini marafiki na majirani. Shaaban Robert anaamini kabisa rafiki na jirani ni

sawa sawa na watu wa nasaba moja endapo tu watu hawa wakikaa katika mapenzi ya kujaliana, kuulizana, kusaidiana na hata kutoleana kauli nzuri zinazoweza kuzidisha mapenzi.

4.3.7 Mapenzi ya Nchi

Ili tuweze kuishi vizuri katika nchi zetu, hatuna budi kuwa na mapenzi ya nchi zetu. Wananchi wanapokuwa hawana mapenzi na nchi zao, basi nchi inakosa thamani, uvunjifu wa amani, chuki zinazaliwa na uhasama unakithiri. Kitendo cha kupenda nchi ni uzalendo, kwa hiyo asiyependa nchi yake hawezi kuwa mzalendo. Hivyo basi, jamii haina budi kupenda nchi ili tuepushe mifarakano na uvunjifu wa amani. Shaaban Robert, ameona umuhimu wake ndiyo maana katika kitabu chake akaweza kulisema jambo hili. Ni vipi wasiyopenda nchi yao wanaweza kufanya shughuli mbalimbali za kuleta maendeleo katika nchi?. Mshairi anasema:

603 Na sisi na nchi zetu
Hatuna miliki zetu
Kwasababu kila mtu
Amehamwa na mapenzi.

4.4 Uchambuzi wa Vipengele vya Fani Katika Kitabu cha Mapenzi Bora

Katika sehemu hii masuala yatakayozungumziwa zaidi ni matumizi ya lugha na muundo wa shairi. Senkoro (1988) anasema kuwa matumizi ya lugha katika kazi ya ushairi ndiyo inayowafanya watu kupenda au kutopenda kazi za mwandishi yeyote wa ushairi wa Kiswahili. Matumizi hayo yapo ya aina kwa aina na huchaguliwa na mtunzi kulingana na ustadi alionao katika utunzi wa mashairi, Senkoro (1988).

Matumizi ya lugha ya ndiyo yanayotawala kwa kiasi kikubwa katika lugha ya mashairi. Ushairi nao ni utanzu wa fasihi ambao hueleza mambo mengi lakini kwa

kutumia lugha ya mkato, mnato na fumbizi kwa wasomaji wake. Hivyo, mtu anapozungumza juu ya lugha za kitamathali katika mashairi hana tafauti na mtu anayezungumzia umuhimu wa maji ya bahari au mto kwa samaki.

Mshairi Shaaban Robert ni mmoja wa washairi nguli wa mashairi ya Kiswahili ambao wanaheshimika sana kimataifa. Miongoni mwa tamathali alizotumia Shaaban Robert katika *Mapenzi Bora* ni tashibiha, takriri, tashihisi, sitiari, kejeli, taswira na nyinginezo.

4.4.1 Matumizi ya Tashibiha

Tashibiha ni tamathali za usemi ambazo hutumika kulinganisha vitu viwili ambavyo havifanani kwa kutumia maneno kama vile; mithili ya, sawa sawa na, mshabaha na, (Njogu na Chimerah,1999). Katika tashibiha ndiyo kunakuwa na dhamira ambazo zimelengwa kuwafikia wasomaji au wasikilizaji wa kazi ya fasihi iliyo mbele ya hadhira.

Shaaban Robert katika *Mapenzi Bora*, sehemu kadhaa ametumia matumizi ya tashibiha:

46 Mapenzi kwangu uhai
Kila mara hukinai
Kama ninywae divai
Baridi katika kuzi.

86 Mapenzi kwa mwanadamu
Kama mshipa na damu
Na mfupa kwa shahamu
Au mti na mzizi.

Hizo beti mbili ni miongoni mwa beti zinazoenyesha tashibiha katika kitabu hiki cha Shaaban Robert, maneno kama ninywae divai katika ubeti wa 46 na kama mshipa wa

damu katika ubeti wa 86 zote zinaonyesha matumizi ya tashibiha kwa kushabihisha umuhimu wa mapenzi kwa mwanadamu ni kama mshipa wa damu, kwani mwanaadamu iliaweze kuwa hai basi lazima awe na damu na damu haiwezi kufanya kazi kama haipo katika mishipa yake maalumu.

Halikadhalika kukosekana kwa mapenzi katika nyumba au jamii basi mambo mengi ya hatari yanaweza kuibika, mfano uchochezi, uhasama, chuki, usaliti na uvunjifu wa amani.

4.4.2 Matumizi ya Takriri

Matumizi ya takriri huifanya hadhira ya kazi ya ushairi kuwa makini na zingativu katika usomaji wao, na hii ni kutokana na nguvu ya takriri katika moyo wa msomaji. Shaaban Robert, katika kitabu chake hiki ametumia takriri sehemu kadhaa katika kusisitiza hadhira kutokana na masuala fulani:

24 Yana ajabu maisha
Yakikaribia kwisha
Ndipo yanapoamsha
Fani **mashazi mashazi**

89 Tutafute tuyaone
Tugawane **tone tone`**
Na yatutibu tupone
Maradhi yenye chukizi.

Katika ubeti wa 24 neno mashazi mashazi ni takriri yenye maana kwa wingi sana na katika ubeti wa 89 tone tone ni takriri iliyojirudia ili kuweka msisitizo kwa hadhira, tone tone ana maana kwa kuonyesha umuhimu wa mapenzi, basi yatafutwe kisha watu wagawane hata kidogo kidogo ili mradi yatibu maradhi mabaya ya chuki, na hapo ameonesha umuhimu wa kuwapo mapenzi katika jamii.

4.4.3 Matumizi ya Tashihisi

Shaaban Robert, katika kitabu cha *Mapenzi Bora* ,pia matumizi ya tashihisi ameyazungumzia sehemu mbalimbali kwa kuwapa sifa za binaadamu,vitu na viumbe visivyo uhai ili mradi tu aweze kufikisha ujumbe kwa hadhira. Miongoni mwa beti zenye tashihisi ni hizi zifuatazo:

132 Chuki ina **uharabu**
Mama wa kila **aibu**
Hata hapewa **dhahabu**
Kuchukuwa ningeizi.

341 Mapenzi yetu hafifu
Ndiye mama yake **hofu**
Na baba wa **upotofu**
Wazazi wa ubaguzi.

Katika beti ya 132 na beti ya 341, maneno uharabu, aibu, hofu, upotofu na ubaguzi ni sifa anazostahili kuwa nazo binaadamu. Mshairi Shaaban Robert ili afikishe ujumbe kwa hadhira yake, ametumia mbinu hii kwa kuipa sifa hizi chuki,na hatimaye ujumbe umefika kwa hadhira kama alivyokusudia. Ameonyesha ubaya wa kukithiri kwa chuki na ameonyesha jinsi gani kukosekana kwa mapenzi kunavyoweza kusababisha kuwepo kwa ubaguzi.

4.4.4 Matumizi ya Sitiari

Kama ilivyoelezwa maana ya sitiari, katika sura ya pili ya mapitio ya kazi tangulizi, ni kauli ya usemi unaotumika kufananisha viti viwili au zaidi bila ya kutumia maneno kama mithili, mfano na kadhalika.

Shaaban Robert, katika kitabu hiki cha *Mapenzi Bora*, matumizi ya sitiari ameyatumia sana ili kufikisha ujumbe kwa hadhira na kuweza kuipamba kazi yake.

Zifuatazo ni beti zenye sitiari:

62 **Mapenzi kwangu kileo**
Cha thamani hata cheo
Ni kinywa hutunza moyo
Josho langu la kutunzi.

240 **Mapenzi pambo moyoni**
Kwa wafupi wastani
Na warefu makundini
Raisi na wanagenzi.

Katika ubeti wa 62 maneno “Mapenzi kwangu kileo”, mshairi ameyafananisha mapenzi na kileo chenye thamani kubwa au cheo. Na katika ubeti wa 243 maneno “Mapenzi pambo la moyo”, mtunzi amefananisha mapenzi na pambo katika moyo, lakini hii yote ni kwa ajili ya kutaka jamii ielewe umuhimu na thamani ya mapenzi katika sehemu husika. Hii ni sawa na kusema, asiyekuwa na mapenzi katika moyo wake sawasawa na kuwa moyo wake hauna pambo, haupendezi na wala hauvutii. Kwa kutumia sitiari katika kitabu chake, anajitahidi kuishawishi jamii kumiliki mapenzi katika moyo.

4.4.5 Matumizi ya Kejeli

Kama maana ya neno kejeli inavyoonyesha katika sura ya pili ni kubeza au kuponda. Katika kitabu cha *Mapenzi Bora*, baadhi ya beti zimeonyesha matumizi ya kejeli. Nazo ni kama hizi zifuatazo:

340 Ulimwengu wa **majini**
Ama watu wenye dini
Wenyeji ni **mashetani**
Ama pepo ya wapenzi.

342 Fedheha kubwa kusema
Chuki iliyo kwa uma

Afadhali ya **wanyama**
Hayawani wa ujuzi.

Katika beti hizi mbili, maneno majini, mashetani, wanyama na hayawani ni maneno ya kejeli ambayo Shaaban Robert ameyatumia kwa ukali sana katika kuikemea jamii ambayo sasa inaonekana mbaya kuliko hata wanyama. Kwa sababu siku zote binaadamu ndiye msikivu, lakini sasa binaadamu amekuwa mkaidi kiasi kwamba haujulikani kama ulimwengu wa watu au majini. Hivyo anaitaka jamii ibadilike na idumishe upendo.

4.4.6 Matumizi ya Taswira

Taswira kama ilivyoelezwa katika sura ya pili, ni maneno yaliyopangwa katika shairi ambalo huweza kuchora picha kamili ya kitu, hali, wazo, dhana au mawazo mengine. Mtunzi Shaaban Robert, katika kufanikisha kazi yake, ametumia sana matumizi ya taswira ili hadhira iweze kuona picha za ujumbe uliobebwa. Hivyo basi ,mtu huguswa moja kwa moja kama vile analiona hilo jambo. Baadhi ya beti zinazoenyesha taswira ni hizi zifuatazo:

679 Wenye moyo wa kutenda
Wape moyo wa kupenda
Wawezeshe na **kupanda**
Maghorofa ya ujuzi.

185 Moyo uwe **bustani**
Mapenzi **yamee** ndani
Tuwe na matumaini
Baraka zile na hizi

Taswira zinazopatika katika beti ya 679 ni maghorofa na kitendo cha kupanda, kwamba mwandishi amekusudia wale walio na moyo wa mapenzi ambao ni

binaadamu basi Mwenyezi Mungu awajaalie kheri, baraka na mafanikio katika kazi zao.

Katika ubeti wa 185, maneno bustani na yamee yanaonyesha taswira ambazo mwandishi amekusudia moyo huo ambao utakubali kumiliki mapenzi basi uwe na wingi wa mapenzi ya kweli na ya kudumu ili kuwe na baraka.

4.5 Muundo/ Umbo la shairi

Muundo ni kipengele cha fani kinachorejelea mpangilio katika kazi ya sanaa ya kifasihi (Njogu na Chimerah,1999). Muundo hujitokeza kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na muundo wa moja kwa moja, muundo rejeshi, muundo changamano na muundo tata. Matumizi ya miundo hii hutegemea uwezo na ujuzi wa mtunzi na huweza pia kutumia pia muundo zaidi ya mmoja katika kazi yake. Katika taaluma ya ushairi, muundo hurejelea namna beti za shairi zilivyoundwa kwa kuzingatia idadi ya mistari iliyotumika kuunda beti za shairi husika.

Katika umbo la shairi la *Mapenzi Bora*, tunaangalia jinsi shairi lilivyoundwa kwa kuzingatia mizani, vina, mishororo na kituo.

4.5.1 Idadi ya mshororo katika ushairi wa Mapenzi Bora

Idadi ya mshororo katika ushairi huu wa *Mapenzi Bora* ni kwamba kila ubeti una mishororo minne yenye mizani 8, kwasababu ushairi huu upo katika aina ya utenzi, tenzi hii ipo katika mashairi ya kimapokeo yenye muundo wa tarbia. Huu ni muundo ambao umetumiwa na watunzi wengi wa mashairi na tenzi. Muundo huu ni rahisi sana kuimbika na ndiyo maana watunzi wengi wa mashairi ya kimapokeo hupenda

kutumia muundo huu. Shaaban Robert na Amri Abedi (1954) wanasema, zipo bahari tatu za ushairi nazo ni: wimbo, shairi na utenzi. Ufuatao ni mfano wa ubeti katika kitabu cha *Mapenzi Bora*, ambao unaonyesha idadi ya mishororo:

180. Mapenzi huunga mbingu
Ardhi na walimwengu
Mbele ya hasimu wangu
Huweza kunipa enzi.

Hivyo basi, kila ubeti una mishororo minne, mfano katika huo ubeti wa juu ambao nauainisha kama ifuatavyo:

Mapenzi huunga mkono-1
Ardhi na walimwengu - 2
Mbele ya hasimu wangu-3
Huweza kunipa enzi -4

4.5.2 Vina na mizani katika ushairi wa Mapenzi Bora

Katika kitabu hiki Shaaban Robert ametunga kazi yake kwa kutumia vina vinavyofanana kwa kila beti na mizani nane kwa kila beti, ambayo imeweza kusaidia kuimbika na kuweka msisitizo kwa hadhira kwa kile alichokusudia na zaidi shairi linakuwa na ladha fulani kama mfano unavyoonekena:

161. Hupendeza kuwa nayo
Mapenzi ua la moyo
Ambao hauna choyo
Wala feli za ushenzi.

Katika ubeti huu, kwa kila mshororo mwisho kuna silabi “yo” ni vina na kila mshororo una mizani 8. Mfano wa mizani katika mshororo wa kwanza:

Hu pe nde za ku wa na yo

1 2 3 4 5 6 7 8

4.5.3 Kituo Katika Ushairi wa Mapenzi Bora

Katika ushairi wa *Mapenzi Bora*, kwa vile ni ushairi wa aina ya utenzi, kituo chake ni bahari ambacho kwa kila ubeti kimebadilika ila kila ubeti bahari yake imeishia na silabi “zi”, mfano wa kituo:

137 Penye mapenzi mapana
Hasama huwa hapana
Na tuhuma na fitina
Kuja hapo haviwezi.

“Kuja hapo haviwezi” ni kituo bahari – ambayo bahari yake imeishia na silabi “zi” iliyojirudia katika beti zote 700. Kwa maelezo hayo ni kwamba, kila ubeti katika beti 700 ya kitabu hiki cha *Mapenzi Bora* kituo bahari chake tofauti lakini kimeishia na silabi “zi”.

4.6 Hitimisho

Katika sura hii uwasilishaji na uchambuzi wa data umefanywa kulingana na madhumuni mahsusi ya utafiti unaosema, “ Kuchunguza dhamira za mapenzi na fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora*”. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa mshairi Shaaban Robert amesawiri dhamira kuu ya mapenzi katika kitabu chake cha *Mapenzi Bora*, ambazo dhamira hiyo ya mapenzi mtafiti ameainisha katika mafungu saba zikiwemo mapenzi ya Mungu, mapenzi ya mitume, mapenzi ya sisi kwa sisi, mapenzi ya majirani na ndugu, mapenzi ya kudumu na mapenzi ya nchi.Uwepo huu wa dhamira ya mapenzi uliyoainishwa katika makundi mbalimbali inathibitisha wazi kuwa kuna hazina kubwa ya vipengele vya kifani vilivyosaidia kuwepo kwa dhamira hiyo na hatimae hadhira kupata ujumbe.

SURA YA TANO

5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho ambayo katika utafiti huu imekusudiwa kutolewa muhtasari, hitimisho na mapendekezo mbalimbali kuhusiana na tafiti za sasa na hapo baadae. Muhtasari wa malengo mahsusi yatatolewa moja baada ya lingine ili kuona matokeo ya utafiti. Sambamba na hilo pia mapendekezo ya utafiti

yatatolewa kwa wahusika mbalimbali ili iwe ni njia moja wapo ya kukuza kazi za fasihi ya Kiswahili kwa ujumla.

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni mahususi matatu ambayo ni kuainisha dhamira za mapenzi katika kitabu cha *Mapenzi Bora,* kuchambua dhamira zilizojitokeza katika kitabu cha *Mapenzi Bora* na kuchunguza vipengele vya fani katika kitabu cha *Mapenzi Bora*. Malengo haya matatu yametimizwa katika uwasilishwaji na uchambuzi wa mjadala wa data za utafiti uliyofanywa katika sura ya tatu na ya nne katika tasnifu hii.

5.2.1 Kuainisha Dhamira Zilizojitokeza Katika Kitabu cha Mapenzi Bora

Dhamira kuu katika ushairi huu ni dhamira ya mapenzi ambayo ndiyo imetawala kitabu kizima. Shaaban Robert anasema, mapenzi ndiyo kila kitu katika maisha ya mwanadamu, bila ya mapenzi katika jamii, mambo mengi mabaya yanaweza kuibuka. Anaendelea kueleza katika beti hizo, mapenzi yanapokosekana basi

uhasama, chuki, ubaguzi, husuda na uvunjifu wa amani lazima vitatokea. Anasema ni vipi mwanaadamu unaishi pasipo na hata chembe ya mapenzi katika moyo wako? Yeye yupo tayari kwa lolote lakini ataendeleza kudumisha mapenzi, na kamwe hawezi kuyaondosha mapenzi nafsini kwake. Zaidi ameelezea sifa na faida za kuwepo kwa mapenzi katika jamii. Anasisitiza kila mtu lazima awe na mapenzi bila ya kuangalia jinsi ulivyo:

238 Yaenee kila nyumba
Kwa wanene na wembamba
Watu wote kuwapamba
Tamthili ya mavazi.

Lakini pamoja na hayo, kuna dhamira kadhaa za mapenzi zilizojitokeza kutokana na utafiti huu. Miongoni mwa uainisho wa dhamira hizo ni pamoja na mapenzi ya Mungu, mapenzi ya mitume, mapenzi ya sisi kwa sisi, mapenzi yasiyoangalia kabila , taifa wala rangi, mapenzi ya kudumu, mapenzi ya majirani na marafiki na mapenzi ya nchi.

5.2.2 Uchambuzi wa Dhamira Zilizojitokeza Katika Kitabu cha Mapenzi Bora

Katika sehemu hii, mtafiti ameweza kuchambua dhamira za mapenzi alizoziainisha kuanzia ya kwanza hadi ya saba. Shaaban Robert amesisitiza mapenzi ya kumpenda Mungu kwasababu ni mapenzi yasiyo na majuto, mawazo, uongo, usaliti wala uongo. Zaidi ya hayo kama mwandishi alivyosema kwamba mapenzi ya kumpenda Allah basi tutapata fungu, yaani tutapata baraka ama thawabu. Mapenzi mengine ni mapenzi ya kuwapenda mitume ambao wao wana mapenzi ya kweli, uvumulivu na subira kama tunavyoona katika historia za mitume wote, hivyo mtunzi wa kitabu amesisitiza kufuata nyayo za mitume katika mapenzi kama inavyoonekana katika

ubeti wa 121. Mapenzi ya kupendana sisi kwa sisi pia yamesisitizwa na mandishi wa *Mapenzi Bora* kwa kusema, tupendane ili tuweze kuondoa chuki na tofauti miongoni mwetu, maneno hayo yapo katika ubeti wa 123. Mapenzi yasiyoangalia kabila, taifa wala rangi, mapenzi ya kupenda nchi, mapenzi ya marafiki na majirani na mwisho mapenzi ya kudumu ambayo ya kupendana katika shida raha.

5.2.3 Uchunguzi wa Vipengele vya Fani Katika Kitabu cha Mapenzi Bora

Katika sehemu hii,inaonyesha dhumuni la tatu la utafiti huu, ambalo vipengele vya fani vimewezwa kuangaliwa kwa utaratibu maalumu. Miongoni mwa vipengele vilivyoangaliwa ni tamathali za usemi zikiwemo tashihisi, tashibiha, takriri, kejeli, sitiari na taswira. Pamoja na hayo ,umbo la shairi limeangaliwa ikiwa ni muundo wa shairi, idadi ya mishororo, vina na mizani pamoja na bahari au kituo. Sehemu hii zaidi imeonesha ufundi aliyoutumia Shaaban Robert katika kufikisha ujumbe kwa hadhira.

5.3 Mapendekezo

Sehemu hii imetoa mapendekezo kutokana na mada. Mtafiti amependekeza mapendekezo yafuatayo:-

5.3.1 Mapendekezo kwa Wasomaji na Jamii kwa Ujumla

Mtafiti anapendekeza kuwa, kila msomi na jamii kwa ujumla kupenda kusoma kazi zote za Shaaban Robert hususani kitabu hiki cha *Mapenzi Bora* ili kuweza kujifunza mengi ambayo si rahisi kuyapata au kujifunza pasipo kusoma kwa umakini kitabu hiki. Jamii itaweza kujifunza ustaraabu, utu na maadili mema ya kuishi kwa amani.

5.3.2 Mapendekezo kwa Serikali

Mtafiti anapendekeza kuwa, serikali ifanye juu chini kwa kuona umuhimu wa maudhui yaliyomo katika kitabu hiki na kuelekeza Wizara ya Elimu kuona umuhimu wa kitabu hiki kusomwa katika vyuo na shule za sekondari ili kujenga taifa jipya lenye upendo wa dhati na amani.

5.3.3 Mapendekezo kwa Watafiti

Mtafiti anapendekeza watafiti wajao wakitafiti zaidi kitabu hiki cha *Mapenzi Bora*, hasa katika kuangalia vipengele vya fani kwa undani zaidi na kulinganisha kitabu hiki cha *Mapenzi Bor*a na vitabu vingine.

MAREJELEO

Babbie, E. (1999). *The Basic of Social Research*. Belmont: Wadsowth.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi Katika Riwaya za Shaaban Robert*, Dar es Salaam: TATAKI.

Escartpit, R. (1974). *Socialogy and Literature*, London: Frank Cass and Co.

Kezilahabi, E. (1976a). *Ushairi wa Shaaban Robert*. East African Literature Bureau.

Kezilahabi, E. (1976b). *Shaaban Robert Mwandishi wa Riwaya*. Tasnifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Kezilahabi, E. (1983). *Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili,* katika makala ya

Kombo, D. K. & Tromph, D. L. A (2002). *Proposal and Thesis Writing –An Introduction*, Nairobi: Paulines Publications.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology*: *Method and Techniques.* New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology*: Methods and Techniques: New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Lakoff, G. & Johnson, M. (1980). *Metaphor We Live,* Chicago: Chicago University Press Ltd.

Maganga, (1971). *Maisha ya Shaaban Robert na mawazo yake. K atika Uchambuzi wa Mawazo ya Kiswahili*. Nairobi: OUP.

Momanyi, C. (2001). *Nadharia ya Uchanganuzi Nafsia Katika Mtazamo wa Kike na Uhakiki wa Kifasihi: Kioo cha Lugha.* Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Tanzania.

Msokile, M. (1993). *Uchambuzi wa Uhakiki: Karibu Ndani*, Dar es Salaam: OUP.

Mulokozi, M. M. & Kahigi, K. K. (1979), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi, M. M. & Sengo, T. S. Y. (1995). *History of Kiswahili Poetry (A.D 1000-2000).* Dar ea Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Mulokozi, M. M. (1982). *Protest and Resistance in Swahili Poetry*: 1600-1885, In Kiswahili Vol. 49(1), Dar es Salaam: TUKI.

Newman, W. L & Wenzake. (2006). *Social Research.* Sixth Edition, Boston: Pearson.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundatiuon.

Omary, M. (2010). Riwaya ya Kiswahili ya Majaribio: Uhakiki wa Ishara, Taswira, Picha na Sitiari Katika Riwaya ya Nagona. Makala ya

Omary, M. (2011). Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa Karibu Ndani (1988) na Dhifa (2008).Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Robert, S. (2008). *Siku ya Watenzi Wote*. Dar es Salaam: TUKI.

Sanka, S. M. (1994). Semantic Deviation in Iraq Oral Poetry. Unpublished M.A Dissertation, University of Dar es Salaam, Tanzania.

Semi za Kimataifa za Kiswahili namba 3.Dar es Salaam: TUKI.

Semina Haijachapishwa.

Sengo, T. S. Y. (1975). *Shaaban Robert: Uhakiki wa Maandishi Yake,* Nairobi: Fondation Books.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: DUP

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Nathari na Tahakiki.* Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F. E. M. K. (2006). Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio Makutano juu ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi*",* Katika *Kioo cha Lugha,* 1, 61-65. Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Topan, F. (1974). *Utangulizi katika Kichomi.* Nairobi: Heinemann.

Twaib, A. H. (2009). Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa Yake. *Mulika,* 130-147. Dar es Salaam: TUKI.

Wamitila, K. W .(2008). *Kanzi ya fasihi* Nairobi: Vide – Muwa.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Lulu za lugha, Kamusi ya Misemo na Nahau.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Kifasihi.* Nairobi: Vide-Muwa.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake,* Nairobi: Phoenix.

Warren, A. & Wellen, R. (1985). *Theory of Literature*. London: Penguin Group.

Young, P. V. (1984). *Scientific Social Services and Research*, Enalewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.